

Ofsi ya IUCN (muungano wa uhifadhi duniani) ya afrika mashariki na kusini, pamoja na CORDIO (shirika la utafti na maendeleo ya pwani na bahari ya hindi) na EAWLS(shirika la afrika mashariki la viumbe hai porini) ziliandaa warsha mbili za jamii mwaka 2007/2008 nchini Kenya na Tanzania. Wakilishi wa jamii waliakisi na kuelezea hadhi ya mazingira ya bahari na kutoa mapendekezo thabiti ya kufanikisha rasilimali za bahari na uendelevu wa chuma riziki. Uchapishaji wa brosha hizi ni matokeo ya kazi hiyo.

Warsha za jamii ni sehemu mojawapo ya mradi mkubwa "uhifadhi kiini cha mali kwa chuma riziki katika afrika mashariki" unaofadhiliwa na IDRC (kituo cha kimataifa cha utafti na maendeleo) na Ford Foundation. Pia mradi wa kujenga uwezo na kuimarisha sera za kuwaezesha jamii ya pwani kusimamia rasilimali zao za bahari katika afrika mashariki unaofadhiliwa na KNCF (mfuko wa fedha wa Kiedanren wa kuhifadhi viumbe). Madhumuni ya miradi hii ni kuongeza maarifa na ufahamu juu ya uhifadhi wa bioanuai unavyochangia chuma riziki na kuwasaidia jamii kudhihirisha umuhimu huu kwa wanasiasa na waundaji sera.

## Kujenga Uwezo wa Jamii Kusimamia Rasilimali ya Baharini Tanzania

# Kundi la Kilimo cha Mwani

# Utangulizi

| | |
|---|---|
| KAMATI ZA USIMAMIZI MTANGA'TA – SAHARE Tanga | • Idihinisha ustawi wa mtandao wa kuhifadhi wa jamii<br>• Kuimarisha chuma riziki kwa jamii kupitia upunguzaji wa uharibifu wa maliasili za bahari<br>• Kupunguza na kuondoa umaskini miongoni wa jamii |
| SHIRIKA LA WAKULIMA WA MWANI KIJIRU LTD Tanga | Tumainisha kamati ? ishchc K Ţ |

1. Biashara ya mwani ina ukiritimba. Uhodhi wa wanunuzi umechangia mashirika machache tu kupewa leseni na kuidhinishwa na serikali ya Tanzania. Leseni hizi zinatumika sehemu maalum peke yake.

2. Ukiritimba wa mashirika umeweka na kusababisha bei kuwa chini na sisizo thabiti.

3. Serikali ya Tanzania haijatambua kilimo cha mwani kama kitega uchumi mbadala. Kwa hivyo, haijatilia mkazo na kuweikwa katika mipango yake ya maendeleo ya serikali.

4. Tuna ukosefu wa pembejeo muhimu za kuimarisha kilimo cha mwani.

5. Tuna mgogoro na wavuvi juu ya zana haramu za wavuvi kama vile sumu, juya na mashua zinazoharibu ugwe wa mwani.

6. Mabadiliko ya hali ya anga yanayoleta mvua nyingi.

